

HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA MTWARA
Simu Na. 023 2410030
Nukushi.023 2410030



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P. 03,
TANDAHIMBA
31/Oktoba/2022

Barua pepe: ded@tandahimbadc.go.tz
Tovuti: www.tandahimbadc.go.tz

TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI NA WAJUMBE WA BODI YA MFUKO WA ELIMU WA WILAYA YA TANDAHIMBA(MARUDIO)

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba anawatangazia wananchi na wakazi wa Wilaya ya Tandahimba nafasi 1 ya Mwenyekiti na nafasi 2 za wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

2.0. NAFASI MOJA (1) YA MWENYEKITI WA BODI

2.1 Sifa za mwombaji

- (i) Awe raia wa Tanzania,
- (ii) Awe na umri usiopungua miaka 25 na asizidi 70,
- (iii) Awe na akili timamu,
- (iv) Awe na elimu ya Chuo Kikuu (angalau Shahada ya kwanza)
- (v) Asiwe na madaraka yoyote kwenye chama cha siasa.
- (vi) Asiwe mtumishi wa Halmashauri.

3.0 NAFASI MBILI (2) ZA WAJUMBE WA BODI

3.1 Sifa za mwombaji

- I. Awe raia wa Tanzania,
- II. Awe na umri usiopungua miaka 25 na asizidi 70,
- III. Awe na akili timamu,
- IV. Awe na elimu ya sekondari, yaani angalau kidato cha nne na kuendelea.
- V. Asiwe na madaraka yoyote kwenye chama cha siasa
- VI. Asiwe mtumishi wa Halmashauri.

4.0 Kazi na majukumu ya bodi ya mfuko wa Elimu zitakuwa kama ifuatavyo:-

- (a) Kubuni Mipango na Mikakati kwa ajili ya maendeleo ya elimu katika Halmashauri.
- (b) Kusimamia mgawanyo wa fedha kwenye shule kufuatana na bajeti iliyoidhinishwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa Bodi na kuridhwa na Baraza la Halmashauri.
- (c) Kusimamia utekelezaji na kutathmini Mipango ya Elimu katika Halmashauri.
- (d) Kujadili na kurekebisha Mipango na Bajeti ya Elimu na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Utendaji kwa ajili ya kuidhinishwa;
- (e) Kupokea, kuchambua na kuidhinisha taarifa za utekelezaji wa Mfuko wa Elimu wa Halmashauri;
- (f) Kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato na rasilimali za kutosha kuendesha Mfuko wa Elimu wa Halmashauri;
- (g) Kushirikiana na Kamati ya Huduma za Jamii ya Halmashauri;
- (h) Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya elimu katika Halmashauri kulingana na programu za kitaifa.
- (i) Kupitisha Kanuni za Utengaji na Utumiaji wa Fedha kutoka kwenye Mfuko kwa ajili ya kuendeleza madhumuni ya Mfuko.
- (j) Kusimamia ujenzi wa shule za Msingi, Sekondari na vyuo vya kati katika Halmashauri.
- (k) Kufanya jambo lolote litakalofanikisha maendeleo ya Elimu katika Halmashauri.

Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza na yatumwe kwa anwani ya, Mkurugenzi Mtendaji(W), S.L.P 03, Tandahimba kwa njia ya posta au kwa kuleta mwenyewe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kabla au ifikapo tarehe 13/11/2022 saa 9:30 Mchana.

NB. Nafasi hizi hazina mshahara wala posho ya mwezi ila kutakuwa na posho ya vikao vya bodi.

Mussa L. Gama
Mkurugenzi Mtendaji (W)
Tandahimba.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P. Box 03
TANDAHIMBA